BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 27 Septemba, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo kwa mwaka 2023/2024.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo kwa mwaka 2023/2024.

III. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

44. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Operesheni nyingi za Jeshi la Polisi katika kukinga, kuzuia na kutokomeza vitendo vya kihalifu zinakosa ufanisi kutokana na uhaba au ukosefu wa mafuta.

Ni lini Serikali itaandaa utaratibu maalumu wa kuipatia ufumbuzi changamoto hiyo.

**Ofisi ya Rais, Ikulu:**

167. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

(a) Ni kiasi gani cha fedha taslimu mpaka hivi sasa zimepatikana kutokana na michango ya Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi.

(b) Je, michango hiyo imetumika vipi katika miradi mbali mbali ya maendeleo ya nchi yetu.

(c) Je, tathmini iko vipi juu ya matarajio ya kukuwa kwa kiwango hicho cha fedha, sambamba na ushiriki wao katika miradi ya maendeleo ya nchi yao.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

17. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na mchakato wa kuandaa Hesabu za Mwisho wa Mwaka kwa taasisi zake zote kwa pamoja (Consolidated Financial Statements).

Je, mchakato huu umefanikiwa wapi.

18. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2022, imeonesha ongezeko la idadi ya watu nchini.

Ni kwa kiasi gani ongezeko hilo linakwenda sambamba na ongezeko la walipakodi waliosajiliwa nchini.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

120. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ni lini hasa suala la kuzagaa ovyo mifugo mitaani na kuathiri vipando, bustani na konde za watu litadhibitiwa licha ya kauli na ahadi nyingi kutolewa bila ya mafanikio.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

177. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Serikali imejitahidi sana kutoa misaada na mikopo nafuu mbali mbali kwa vijana ili waweze kujinasua na umasikini.

Ni lini Serikali itawekeza kwenye elimu ya ukombozi wa kifikra ili vijana waweze kujinasua na hali ngumu ya maisha.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

270. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Bodi ya ligi kuu Tanzania bara imetangaza kuanza kuvitumia Viwanja vya Amani Complex na Gombani kwa baadhi ya mechi za ligi hiyo. Pamoja na fursa hii nzuri kwa Zanzibar, yapo malalamiko mengi kutoka kwa wadau wa soka nchini.

(a) Ni kwa kiasi gani uchezaji huu wa ligi kuu ya Tanzania bara hapa Zanzibar hautaua moja kwa moja ligi ya Zanzibar.

(b) Ni upi mkakati wa Serikali wa kuitafutia udhamini ligi ya Zanzibar ili iwe bora kama ligi ya Tanzania bara.

(c) Je, Serikali ina mkakati wowote wa kuiwezesha ligi ya wanawake ya mpira wa miguu hapa Zanzibar.

278. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Tunaipongeza Serikali kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) kwa juhudi zake za kuonesha Baraza la Wawakilishi mubashara (live) katika vikao vyake vya kila siku. Pamoja na pongezi hizi, kumekuwa na malalamiko juu ya ubora (quality) wa mifumo ya urushaji wa matangazo hayo ukilinganisha na mifumo ile inayotumika katika vyombo vyengine vya habari.

(a) Je, Serikali inalishughulikia vipi suala la ubora hafifu wa mifumo na kamera zinazotumiwa na ZBC kurushia matangazo haya ya Baraza.

(b) Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuliwezesha Shirika hili kuweza kurusha matangazo kwa mifumo ya kisasa na yenye ubora mkubwa.

**<u>Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto :</u>**

165. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Tathmini iko vipi juu ya usawa wa kijisia katika suala zima la uongozi na ajira mpaka sasa.

166. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Je, Serikali haioni kwamba kwa sasa upo umuhimu wa kuwapatia wazee wenye mahitaji maalumu, gawio maalumu la kuwawezesha kujikimu kama ni ziada ya kuzijali hali zao.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

275. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya

Pamoja na juhudi kubwa za Serikali za kuimarisha hospitali za Zanzibar, bado kuna uhaba mkubwa wa Wataalamu wa Dawa za Usingizi na Ganzi (Anesthesia), jambo linaloathiri utendaji na utoaji wa huduma za upasuaji.

(a) Je, ni Wataalamu wangapi wa Usingizi na Ganzi ambao hivi sasa wanatoa huduma hiyo kwa hospitali za umma.

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa muda mrefu wa kutatua tatizo la uhaba wa Wataalamu hao.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

104. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Ni ipi nafasi ya zao la shelisheli katika uhitaji wa ndani kibiashara na uhitaji wa soko la kimataifa.

(b) Tathmini iko vipi juu ya idadi ya mishelisheli kwa muktadha wa kuongezeka na kupungua kwake.

(c) Ni ipi faida ya zao hili kiafya.

106. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Tathmini ya uzalishaji na ubora wa asali inayozalishwa na wajasiriamali tofauti Zanzibar ipo vipi kwa sasa.

(b) Kwa kiasi gani uzalishaji wa zao la asali umeanza kufungua sura mpya ya uhitaji katika soko la kitaifa na kimataifa.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**27 Septemba, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**